

Jibu: Msiche linatokana na Neno “kucha/kumcha”.. Na maana ya Neno “Kucha” ni “kuhofu”.

Hivyo mtu anapomwofu “mtu”, maana yake anamcha huyo mtu, na pia anapomhofu MUNGU maana yake anamcha Mungu, na matokeo ya kumcha MUNGU ni kumheshimu, kumtumikia, na kufanya mapenzi yake. Lakini mtu asiyemcha MUNGU basi hawezi kufanya hayo yote.

Vile vile mtu anayemcha mwanadamu mwenzake, tafsiri yake ni kwamba anamtumikia, anamheshimu, anamtii na kufanya yale yote mtu huyo anayomwagiza.

Vile vile mtu anayeicha miungu mingine tofauti na MUNGU wa mbingu na nchi, tafsiri yake ni kwamba anaitumikia ile miungu, na kuihofu na kuitii na kuiheshimu.

Hivyo Neno “msiche” ni kinyume cha “kucha/kumcha” na tafsiri yake ni “kutohofu”

1. Mfano wa mistari unayokataza uchaji wa mtu (kumcha mtu)

*Kumbukumbu 1:17 “Msitazame nafsi za watu katika hukumu; mwasikize wadogo na wakubwa sawasawa; MSICHE USO WA MTU AWAYE YOTE; kwa kuwa hukumu ni ya Mungu; na lile neno liwashindalo mniletee mimi, nami nitalisikiza”.*

Hapo Bwana MUNGU anakataza watu kuhofu wanadamu wenzao.. Na mistari mingine ni pamoja na *Yoshua 10:25*.

2. Mfano wa mistari inayotaja kuicha miungu mingine.

*2Wafalme 17:35 “hao ambao Bwana alifanya agano nao, akawaamuru, akasema, MSICHE miungu mingine, wala kuisujudia, wala kuitumikia, wala kuitolea sadaka*

*37 na sheria, na hukumu, na torati, na amri, alizowaandikia, hizo ndizo mtakazozishika na kuzifanya hata milele; wala msiche miungu mingine.*

*38 Na hilo agano nililofanya nanyi, msilisahau; wala MSICHE miungu mingine”*

3. Mistari inayotaja uchaji wa MUNGU wa mbingu na nchi. (yaani kumcha MUNGU wa mbingu na Nchi).

*Yoshua 24:14 “Basi sasa MCHENI BWANA, mkamtumikie kwa unyofu wa moyo na kwa kweli; na kuiweka mbali miungu ambayo baba zenu waliitumikia ng’ambo ya Mto, na huko Misri; mkamtumikie yeye Bwana.”*

Soma pia *Kumbukumbu 13:4, 1Samweli 12:24, Zaburi 22:23, Zaburi 34:9, 1Petro 2:17, na Ufunuo 14:7.*

Kwa hitimisho ni kwamba biblia imetukataza TUSICHE miungu yoyote wala mwanadamu yoyote, bali TUMCHE BWANA MUNGU MWETU, aliyetuumba.

*Ufunuo 14:7 “akasema kwa sauti kuu, Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja. Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji”*

Je umeokoka?, Je una uhakika BWANA akirudi leo unakwenda naye??... Je huna uhakika huo basi tayari huo ni uthibitisho kuwa akija hutakwenda naye, ni heri ukampokea BWANA YESU LEO, akutakase na kukupa uhakika wa uzima wa milele.

Maran atha.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kupofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

**UNAMFAHAMU MUNGU WA KWELI?**

Neno “Msiche” maana yake nini? (Kumbukumbu 1:17)

Kuna Mbingu ngapi?

Mbinguni ni sehemu gani?

Nini maana ya mbingu na nchi zitapita lakini maneno yangu hayatapita kamwe? (Mathayo 24:35).

**FAHAMU SEHEMU NNE (4) APANDWAPO MWAMINI.**

Rudi Nyumbani

Share on:  
WhatsApp

Print this post